



PreK 4 ME, Uhusiano wa Familia


SOMO LA 2: *RAFIKI*

Muhtasari wa Somo la 2: Rafiki

Mwezi huu tutajifunza kuhusu rafiki zetu, pamoja na jinsi ya kusuluhisha mizozo, maana ya kuwa rafiki mzuri, na kusaidiana na kushirikiana na rafiki zetu darasani— na nyumbani. Tutazingatia jinsi ya kucheza na wanafunzi wenzetu, kushiriki vifaa na kutafuta suluhisho wakati mizozo ya kijamii itatokea.


Tunaanza pia kutambua maneno yenye urari na sauti za kwanza za herufi kupitia nyimbo, mashairi na vitabu. Watoto wataanza kugundua nyenzo za uandishi na kuanza kukuza ujuzi wa uandishi wa kwanza kupitia michezo!

VITABU VYA SPOTLIGHT vya Somo la 2




*The Little Red Hen
Makes a Pizza*

Cha : Philomena Sturges
na Amy Walrod



Matthew and Tilly

Cha: Rebecca C. Jones




A Letter to Amy

Cha: Ezra Jack Keats

Dandelion

Na Don Freeman

Picha zimepakuliwa amazon.com



Vitabu vingine mwezi
huu ni pamoja na:

Shape Capers Cha: Cathryn Falwell

Hooray, A Pinata Cha: Elisa Kleven

Every Buddy Counts Cha: Stewart J Murphy

Nyimbo, Herufi na Kucheza na Lugha

Shiriki wimbo mpya wenye urari ambao tunajifunza darasani mwezi huu, ukifanya zoezi zuri la kuhesabu!

Maembe Matano Matamu

Maembe matano (5) matamu yamehifadhiwa ghalani, (child's name) amekula embe moja, maembe manne (4) yamebakia;

Maembe manne (4) matamu ya manjano, (child's name) amekula embe moja, maembe matatu (3) yamebakia;

Maembe matatu (3) matamu kama asali, (child's name) amekula embe moja, maembe mawili (2) yamebakia;

Maembe mawili (2) matamu na ya kupendeza, (child's name) amekula embe moja, embe moja (1) limebakia;

Embe moja (1) tamu limebakia peke, (child's name) amekula embe moja, hakuna (0) lililobakia!

Mwenye duka, tafadhali agiza mengine—tunapenda kununua maembe tunapokuja dukani mwako!



Image from Pixabay

Angalia sehemu inayofuata uone mazoezi ya nyumbani



Wezesha Masomo ya Nyumbani Kupitia Mazoezi haya ya Ziada

Viwango vya Sanaa, Kusoma na Elimu ya Kijamii

Kutengeneza kadi

Msaidie mtoto wako kutengeneza na kupamba kadi ya kumtumia rafiki! Kata picha kwenye majarida, chora au upake rangi kwenye karatasi tupu ambayo umeikunja katikati. Unaweza kumsaidia mtoto wako kuandika jina la rafiki zake, na hata jina lake-mwenyewe!

Viwango vya Kusoma na mbinu za kujifunza

Zoezi la kutafuta vitu

“Vinavyoanzia Na”

Mwambie mtoto wako atafute vitu ndani au nje ya nyumba ambavyo majina yake yanaanza na sauti za herufi utakazompa. Kwa mfanano, mwambie mtoto wako atafute kitu kinachoanza na sauti ya 'R' ("rrrrrr") Anaweza kutafuta rula. Ikiwa anahitaji usaidizi, mpe chaguo kati ya kalamu na rula.

Viwango vya Lugha na Kusoma, Elimu ya Kijamii na Hesabu

Ziara ya sokoni

Mtaani kwako kuna duka la vyakula au soko dogo? Mwambie mtoto wako akusaidie kuandaa orodha ya vyakula vya kununua kwa kuchora au kukata picha kwenye kipeperushi cha duka. Nunua bidhaa ukiwa na mtoto wako, ukimwonyesha bidhaa mpya, ukimsaidia kutafuta bidhaa zilizo kwenye orodha yake. Tumia maneno ya kufafanua bidhaa hizi: nzito, ngumu, laini, nyepesi, kuelezea vitu. Hesabu bidhaa unazozipata ukiwa na mtoto wako.



Picha imetolewaPixabay

Vidokezo vya Kuzungumza na Kusoma Pamoja

Kuanzisha Mazungumzo:

- Unapenda zaidi sehemu gani ya hadithi hii?
- Ni jambo gani la kwanza linalotokea kwenye hadithi hii?
- Unafikiri ni nini kitatokea baadaye?

Kidokezo kwa Familia na Wazazi : Kwa nini Michezo ni Muhimu?

Maelezo yafuatayo yametolewa kwenye tamthilia ya “10 Things Every Parent Should Know About Play” iliyoandikwa na Laurel Bongiorno, PhD (<https://www.naeyc.org/our-work/families/10-things-every-parent-play>)

Kucheza ni nafasi bora ya watoto kujifunza.

Watoto hufanya mazoezi na kuimarisha kujifunza kwao katika maeneo mbalimbali wakati wa kucheza. Michezo huwapa nafasi na muda wa kujifunza ambao hauwezi kupatikana kupitia kujaza karatasi. Kwa mfanano, katika mchezo wa mkahawa, watoto huandika na kuandaa menyu, kuweka bei, kuchukua oda na kufanya ukaguzi. Michezo hutoa nafasi nzuri sana za kujifunza na huwawezesha watoto kufanikiwa na kujithamini.

Tenga wakati wa kucheza.

Wazazi ndio wahimizaji wakuu zaidi wa kujifunza kwa watoto wao. Unaweza kuhakikisha kuwa wamepata wakati mwingi wa kucheza iwezekanavyo saa za mchana ili kuwawezesha ukuaji wa kiutambuzi, lugha, kimwili, kijamii na kihisia.